

# Kipimo cha haraka cha KUPIMA MALARIA (mRDT)

## Kipimo cha mRDT ni nini?

Ni kipimo cha haraka na cha uhakika cha kupima vimelea vya malaria ambacho kimethibitishwa na serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa jamii


Mara tu unapohisi dalili za malaria, ni muhimu kuwahi kituo cha kutolea huduma ya afya ukapime ili ujue kama una vimelea vya malaria au unasumbuliwa na ugonjwa mwingine.

Serikali imeanzisha kipimo cha uhakika na haraka cha kupima malaria (mRDT. Usitumie dawa za malaria bila kupima. Haya ndiyo mambo ya msingi ya:

- Mara tu uonapo dalili za ugonjwa wa malaria ni muhimu kuwahi kituo cha afya ukapime ili ujue kama una malaria au unasumbuliwa na ugonjwa mwingine
- Mtoa huduma ya afya atachukua damu yako kisha kuiweka kwenye kipimo cha haraka cha kupima malaria (mRDT) na baada ya dakika chache tu atakupatia majibu yako.
- Kama majibu yako yanaonyesha kuwa una vimelea vya malaria, mtoa huduma ya afya atakupatia dawa za malaria. Kwa sasa, dawa ya malaria ni Dawa Mseto.

## Mambo muhimu ya kuifahamisha jamii kuhusu kipimo cha haraka cha kupima malaria (mRDT)

- Usitumie dawa za malaria bila kupima. Mara tu uonapo dalili za malaria, ni muhimu kuwahi kituo cha afya ukapime ili ujue kama una vimelea vya malaria au unasumbuliwa na ugonjwa mwingine.
- Serikali imeanzisha kipimo cha uhakika na haraka cha kupima malaria (mRDT)
- mRDT ni kipimo cha haraka na uhakika cha kupima malaria. Utapatiwa majibu yako baada ya dakika chache tu
- Ni muhimu kuisisitiza kwamba kipimo cha haraka cha kupima malaria (mRDT) kimethibitishwa na serikali kuwa ni sahihi na cha kuaminika
- Iwapo majibu yako yataonyesha kuwa hauna malaria, mtoa huduma ya afya atajadiliana na wewe juu ya mambo mengine ya kufanya ikiwemo kufanya vipimo vya magonjwa mengine au kukuandikia rufaa uende kituo kingine ambapo wataweza kukufanyia vipimo vya ziada.
- Iwapo majibu yako yataonyesha kuwa huna malaria, utafanyiwa vipimo vya magonjwa mengine au utaandikiwa rufaa uende kituo kingine ambapo wataweza kukufanyia vipimo vya ziada.



# Kipimo cha haraka cha KUPIMA MALARIA (mRDT)

